JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**Kumb.Na: EB.32/160/01/199** **16 Disemba, 2024**

Mwenyekiti,
Registered Trustees of Islamic Foundation t/a Radio Imaan,
Barabara ya Korogwe - Msamvu
S.L. P 6011,
**67128 MOROGORO.**

## AMRI YA UTEKELEZAJI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 48 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 ya Sheria za Tanzania)*

1. Tarehe 27 Julai 2021 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (ambayo inarejewa hapa kama "TCRA"), ilitoa leseni ya Huduma za Utangazaji kwa njia ya redio (*Free to Air - Radio*) (ambayo inarejewa hapa kama "Leseni") pamoja na rasilimali masafa ya redio kwa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Uislam (Registered Trustees of Islamic Foundation) t/a Radio Imaan (ambayo inarejewa hapa kama "Mtoa Huduma") kwa ajili ya utoaji wa huduma za utangazaji maeneo ya mikoa ya Morogoro, Arusha, Mwanza, Kigoma, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Tabora, Ruvuma na Dar es Salaam. Pia TCRA ilitoa Kibali cha Ujenzi kwa Mtoa Huduma ili aweze kujenga miundombinu na kufunga mitambo na vifaa mbalimbali kwa ajili ya usambazaji wa mtandao wa redio.

2. Leseni iliyotolewa kwa Mtoa Huduma inamtaka Mtoa Huduma, wakati akitoa huduma, kufuata sheria, kanuni, masharti ya leseni, miongozo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na TCRA.

3. Aya ya tatu (3) ya Masharti ya Kibali cha Ujenzi kilichotolewa kwa Mtoa Huduma inamtaka mmiliki wa kibali cha ujenzi kufunga kifaa cha kuchuja mawimbi (*cavity filter*) chenye uwezo wa kuchuja mawimbi yasiyopungua *70dBc* kwenye kifaa cha kurusha matangazo.

   *"The permit holder shall install cavity filters at the output of its transmitter with isolation (attenuation) of not less than 70 dBc"*

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified

4. Katika kutekeleza majukumu yake ya kiusimamizi, tarehe 17-20 Juni, 2024 TCRA ilifanya ukaguzi katika kituo cha Mtoa Huduma cha mitambo ya usambazaji wa mawimbi kilichopo katika kilima cha Imagi mjini Dodoma, na kubaini kuwa, Mtoa Huduma alikuwa hajafunga kifaa cha kuchuja mawimbi (*cavity filter*) kwenye vifaa vya kurusha matangazo(*transmitter*) kinyume na aya ya tatu (3) ya masharti ya Kibali cha Ujenzi alichopewa na TCRA.

5. Baada ya kubaini ukiukaji huo, tarehe 01 Julai, 2024 TCRA ilitoa maelekezo ya maandishi ikimtaka Mtoa Huduma, ndani ya kipindi cha muda wa miezi mitatu (3), kufuata masharti ya Kibali cha Ujenzi kwa kufunga kifaa cha kuchuja mawimbi (*cavity filter*) katika mitambo yake ya kusambaza mawimbi iliyopo kilima cha Imagi, Dodoma.

6. Baada ya muda wa miezi mitatu (3) kumalizika, tarehe 16 Oktoba 2024 TCRA ilifanya tena ukaguzi katika kituo cha Mtoa Huduma cha mitambo ya usambazaji cha Imagi mjini Dodoma na kubaini kuwa, Mtoa Huduma alikuwa hajatekeleza maelekezo yaliyotolewa tarehe 1 Julai 2024 kwa kutofunga kifaa cha kuchuja mawimbi (cavity filter) kwenye vifaa vya kurusha matangazo(transmitter) kinyume na aya ya tatu (3) ya masharti ya Kibali cha Ujenzi alichopewa na TCRA.

HIVYO BASI; kufuatia ukiukwaji huo TCRA inatoa onyo kwa Registered Trustees of Islamic Foundation kwa kushindwa kutimiza masharti ya kibali cha ujenzi na kukaidi maelekezo ya TCRA, na pia Registered Trustees of Islamic Foundation inaelekezwa:

1. Kuzima vifaa vya kurushia matangazo (Transmitter) katika kituo cha mitambo ya usambazaji wa mawimbi kilichopo katika kilima cha Imagi mjini Dodoma ndani ya siku saba (7) kuanzia tarehe ya Amri hii mpaka pale itakapotekeleza masharti ya kibali cha ujenzi na maelekezo ya TCRA; na

2. Kufunga kifaa cha kuchuja mawimbi (*cavity filter*) kwenye vifaa vya kurushia matangazo(*transmitter*) na kuitaarifu TCRA kwa ajili ya kufanya ukaguzi ili kutoa ruhusa ya kuwasha tena mitambo hiyo.

Endapo Registered Trustees of Islamic Foundation itashindwa, itazembea, au kukataa kutekeleza amri hii, TCRA itaendelea kuchukua hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti dhidi ya Registered Trustees of Islamic Foundation kwa mujibu wa sheria.

Amri hii imetolewa leo tarehe ...20/12... **Disemba, 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Amri hii imetolewa na kupokelewa na **REGISTERED TRUSTEES OF ISLAMIC FOUNDATION** tarehe.......20.......mwezi ....12......, 2024.

Jina: ..MUHAMMAD AREF NAHDI......

Sahihi: ..............................................

Cheo: ...PROJECT DIRECTOR.............

(Muhuri wa Ofisi)

*(Amri hii imetolewa katika nakala mbili (duplicate). Tafadhali weka saini katika nakala zote mbili na ubaki na nakala yako, kisha wasilisha nakala nyingine TCRA kuthibitisha kupokea Amri hii)*

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified